TANGAZO LA SERIKALI NA. 707 la tarehe 02/12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA GOWEKO YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Goweko ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Unaanzia kwenye alama G1 Mashariki ya Makazi ya Goweko katika njia ya reli ya Itigi katika majira - nukta 518520E, 9410556N baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S105$^0$7’0”W kwa umbali wa kilometa 1.9 hadi alama ya mpaka G2 iliyopo barabara ya Kirungi yenye majira-nukta 516636E, 9409810N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S257$^0$17’8”W kupitia barabara ya Kirungi hadi alama ya mpaka G3 yenye majira-nukta 516226E, 9407696N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo W95$^0$6’20” kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi G4 yenye majira-nukta 514469E, 9407790N Kusini mwa makazi ya Nsololo; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa 93$^0$6’12” kwa umbali wa kilomita 1.1 hadi alama ya mpaka G5 iliyopo barabara ya Kawekapina kwenye majira-nukta 514221E, 9408921N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa N257$^0$17’8”E kwa umbali wa kilomita 3.7 hadi alama ya mpaka G6 iliyopo pembezoni mwa reli ya Itigi - Tabora katika majira - nukta 514638E, 9412597N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa N103$^0$6’52”E kwa umbali wa kilomita 1.6 hadi alama ya mpaka G7 iliyopo katika barabara ya Kigwa yenye majira - nukta 516234E,

*Tangazo la serikali na. 707 (linaendelea)*

94013231N; baada ya hapo mpaka unaendelea kuelekea Mashariki katika uelekeo wa E175$^{0}$11̓40̎ kwa umbali wa kilomita 3 hadi alama ya mpaka G8 iliyopo barabara ya Miwitulule katika majira-nukta 519249E, 9413622N; baada ya hapo mapaka unaelekea kusini katika uelekeo wa S86$^{0}$5̓44̎W kwa umbali wa kilomita 2.7 hadi alama ya mpaka G9 iliyopo barabara ya Kamama yenye majira-nukta 518730E,9411516N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa N40$^{0}$2̓40̈ kwa umbali wa kimolita 1.0” hadi ulipoanzia.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*